**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA**

**MTIHANI WA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI**

**711** **KISWAHILI**

**Muda: Masaa 3** **Ijumaa, 06th May 2016 Asubuhi**

---

**Instructions.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A, B** na **C** zenye jumla ya maswali kumi na sit (16).

2. Jibu maswali yote kutoka sehemu A na maswali mawili kutoka kila sehem **B** na **C**.

3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** na **C** Zina jumla ya alama **sitini (60).**

4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.

5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha majibu.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii. Kila swali kina alama 4.

1. (a) Eleza maana ya lahaja.

    (b) Taja lahaja mbili za Kiswahili na eleza eneo moja linalozungumza kila lahaja.

    (c) Eleza umuhimu wa lahaja katika kukuza lugha ya Kiswahili.

    (d) Tofautisha lahaja na lugha.

2. Eleza maana ya viambishi na taja viambishi viwili vya wakati kisha utunge sentensi moja kwa kila kiambishi.

3. Kwa kutumia mifano, eleza tofauti kati ya nomino za pekee na nomino za kawaida.

4. (a) Eleza maana ya uakifishaji.

    (b) Taja alama mbili za uakifishaji na onyesha matumizi yake katika sentensi moja moja.

5. Eleza maana ya kitenzi kikuu na kitenzi msaidizi kisha andika sentensi moja kwa kila aina ya kitenzi.

6. Taja aina mbili za sentensi za Kiswahili kulingana na mtindo wa mawasiliano na toa mfano wa kila aina.

7. (a) Fafanua maana ya methali.

    (b) Eleza tofauti mbili kati ya methali na nahau.

8. Eleza maana ya tamathali ya usemi ya kejeli na toa mfano mmoja wa sentensi inayotumia tamathali hiyo.

9. Kwa hoja mbili, eleza jinsi Kiswahili kinavyoweza kutumika kama chombo cha kueneza elimu kwa jamii.

10. Taja sababu mbili zinazochangia kuharibika kwa lugha ya Kiswahili miongoni mwa vijana wa sasa na eleza athari zake.

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali mawili kati ya manne. Kila swali lina alama 15.

11. Eleza mchango wa wahariri wa vitabu vya Kiswahili katika kukuza lugha ya taifa kwa hoja sita.

12. Kwa kutumia hoja sita, eleza kwa nini baadhi ya wanafunzi hupata ugumu wa kuandika insha za Kiswahili kwa ufasaha.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

13. Jadili kwa hoja sita nafasi ya lugha ya Kiswahili katika kukuza utalii nchini Tanzania.

14. Eleza mchango wa vyombo vya habari katika kuendeleza Kiswahili nchini kwa kutumia hoja sita.

**SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali mawili tu kutoka sehemu hii. Kila swali lina alama 15.

15. Andika insha ya kisimi yenye kichwa: *Tamaa mbele mauti.*

16. Kwa kutumia hoja sita, eleza jinsi ambavyo mashairi ya Kiswahili yanaweza kutumika kama chombo cha mabadiliko ya kijamii.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org